



## HAKIKA ZA HAKIKA KUHUSU

# Bima ya Afya kwa Wahamiaji

NY State of Health ni soko la mtandaoni la mipango ya bima za afya. Kila mtu anafaa kuja kwenye Soko hili ili kuona kile linaweza kutoa.

Haijalishi ulipozaliwa. NY State of Health inaweza kukusaidia.



Mtandaoni katika  
[nystateofhealth.ny.gov](http://nystateofhealth.ny.gov)



Kwa simu kupitia  
1-855-355-5777

TTY  
1-800-662-1220

## Hapa kuna vitu 4 muhimu unafaa kujua kuhusu NY State of Health

### 1 Taarifa unazotupatia hazitashirikiwa

Unachoiambia NY State of Health na washauri wake ni cha faraghani. Taarifa unazotupatia ili kujisajili katika mpango wa bima ya afya hazitashirikiwa na mtu mwingine yeyote. Na hazitatumiwa kwa dhumuni lingine lolote.

### 2 Utapata usaidizi bila kujali jinsi wewe au familia yako ilivyokuja humu nchini

Hata kama hauna karatasi za uhamiaji, au kama jamaa wa familia yako walikuja humu nchini kwa njia tofauti, unahitaji tu kujaza OMBI MOJA kwa kila mtu. Na, na bila kujali hadhi yako, bado unaweza kupata Medicaid ya dharura na bima ya kawaida ya afya kwa watoto wako (Child Health Plus).

### 3 Utapata usaidizi kwa lugha nyingi

- Watu wanaojibu simu zetu wanazungumza lugha nyingi. Ikiwa hawazungumzi lugha yako, watakutafutia mtafsiri.
- Tuna watu waliopitia mafunzo wanaozungumza lugha yako. Ikiwa ungetaka, pia wanaweza kuja mahali unapoishi au unapofanya kazi.

### 4 Utapata usaidizi kwa namna nyingi

Unaweza kupata usaidizi mtandaoni, kwenye simu au ana kwa ana katika jamii yako. Washauri wetu waliopitia mafunzo watakusaidia kupitia kila hatua ya kuchagua na kujisajili katika mpango wa bima ya afya.

- Mtandaoni katika [nystateofhealth.ny.gov](http://nystateofhealth.ny.gov)
- Kwa simu kupitia 1-855-355-5777, TTY: 1-800-662-1220